# GAZETI RASMI LA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

**18 AGOSTI 2026**

***Hupigwa Chapa kwa Idhini ya Serikali na Imekubaliwa na Mkuu wa Posta kuwa ni Gazeti*** ***Hutolewa kila Ijumaa***

***Bei Tshs . 5000/=*** **CXXXV Nam. 7531**

**YALIYOMO** *Ukurasa*

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Chuo cha Fedha Zanzibar, kuweka Masharti ya Utoaji wa Elimu katika Fani za Biashara na Fedha na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo: ...................................................... ..00

## SEHEMU YA SHERIA

Sheria iliyotajwa hapo chini imetangazwa katika ***Gazeti Rasmi*** hili.

### Tangazo la Mswada

**Nam.** Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Chuo cha Fedha Zanzibar, kuweka Masharti ya Utoaji wa Elimu katika Fani za Biashara na Fedha na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo:-

### TANGAZO

Mswada ufuatao utawasilishwa katika Mkutano wa Baraza la Wawakilishi utakaoanza tarehe 9 Septemba, 2026 kwa kusomwa mara ya kwanza na unachapishwa pamoja na Madhumuni na Sababu zake kwa ajili ya kutoa taarifa kwa wananchi.

**ZANZIBAR**
18 Agosti, 2026

(Ndugu Mansura Mosi Kassim)
***Katibu wa Baraza la Mapinduzi***
***na Katibu Mkuu Kiongozi.***

**Matangazo yaliyohusu Waliofariki na Mali wa Watu waliofariki, kuvunja Mikataba ya ushirikiano, taarifa za Makampuni, Upotevu na marekebisho ya Nyaraka za Serikali na mengineyo ambayo ni muhimu kwa Umma lazima kuchapishwa katika Gazeti Rasmi. Nakala za Matangazo hayo zipelekwe kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar - Tanzania SLP 261 Maruhubi, Zanzibar. Nakala ziwasilishwe kabla ya Siku ya Alhanisi ya kila Wiki**

**MSWADA**

*wa*

# SHERIA YA KUANZISHA CHUO CHA FEDHA ZANZIBAR, KUWEKA MASHARTI YA UTOAJI WA ELIMU KATIKA FANI ZA BIASHARA NA FEDHA NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Chuo cha Fedha Zanzibar, 2026 na itaanza kutumika baada ya kutiwa saini na Rais.

Ufafanuzi.

**2.** Katika Sheria hii, isipokuwa kama maelezo yatahitaji vyenginevyo:

"Baraza" maana yake ni Baraza la Chuo lililoanzishwa chini ya masharti ya kifungu cha 7 cha Sheria hii;

"Chuo" maana yake ni Chuo cha Fedha Zanzibar kilichoanzishwa chini ya masharti ya kifungu cha 3 cha Sheria hii;

"Mkuu wa Chuo" maana yake ni Mkuu wa Chuo aliyeteuliwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 13 cha Sheria hii;

"mwanafunzi" maana yake ni mtu yeyote aliyesajiliwa na Chuo kwa madhumuni ya kusoma;

"Naibu Mkuu wa Chuo Taaluma, Utafiti na Ushauri Elekezi" maana yake ni Naibu Mkuu wa Chuo Taaluma, Utafiti na Ushauri Elekezi aliyeteuliwa chini ya masharti ya kifungu cha 17 cha Sheria hii;

"Naibu Mkuu wa Chuo Utawala, Mipango na Fedha" maana yake ni Naibu Mkuu wa Chuo Utawala, Mipango na Fedha aliyeteuliwa chini ya masharti ya kifungu cha 15 cha Sheria hii;

"Rais" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

"Serikali" maana yake ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

"Serikali ya Wanafunzi" maana yake ni Serikali ya Wanafunzi iliyoanzishwa chini ya masharti ya kifungu cha 22 cha Sheria hii;

"tuzo" maana yake ni astashahada, stashahada, shahada na tuzo nyengine ya kitaaluma inayotolewa na Chuo kwa mtu ambaye amefanikiwa kumaliza programu ya masomo; na

"Waziri" maana yake ni Waziri anayehusika na fedha.

## SEHEMU YA PILI
## UANZISHWAJI WA CHUO

Uanzishwaji wa Chuo.

**3.-**(1) Kunaanzishwa Chuo kitakachojulikana kama Chuo cha Fedha Zanzibar na ufupisho wake utakuwa ni "ZIF".

(2) Chuo kitakuwa ni chombo kinachojitegemea, chenye urithi wa kuendelea na muhuri wake na kwa jina lake, kwa mujibu wa sheria, kitakuwa na uwezo wa:

(a) kushtaki na kushtakiwa;

(b) kupata, kumiliki, kununua na kuondosha mali yoyote inayohamishika na isiyohamishika;

(c) kuingia katika mkataba au muamala wowote;

(d) kukopa kiwango chochote cha fedha kutoka katika taasisi yoyote ya fedha; na

(e) kutekeleza au kufanya kitendo au jambo lolote ambalo linaweza kutekelezwa au kufanywa na chombo kinachojitegemea.

Muhuri na nembo ya Chuo.

**4.-**(1) Kutakuwa na muhuri na nembo ya Chuo katika umbo na namna kama itakavyoamuliwa na Baraza.

(2) Matumizi ya muhuri na nembo ya Chuo katika waraka wowote yatathibitishwa na saini ya Mkuu wa Chuo au afisa mwengine yeyote wa Chuo aliyeidhinishwa kwa maandishi na Mkuu wa Chuo.

(3) Waraka wowote unaokusudiwa kuwa ni hati inayotolewa na Chuo utawekwa muhuri wa Chuo na utathibitishwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki.

Kazi za Chuo.

**5.** Chuo kitakuwa na kazi ya:

(a) kutambua mahitaji ya mafunzo ya sekta husika na wataalamu wake katika ngazi mbalimbali;

(b) kuandaa na kupitia mitaala;

(c) kuandaa semina, mikutano na warsha kwa ajili ya kuwajengea uwezo wataalamu katika masuala yanayohusiana na fedha na fani zinazohusiana na hizo;

(d) kuandaa, kupitia na kuendesha programu za mafunzo kwa lengo la kukuza ujuzi katika fani ya uhasibu, ukaguzi, benki na fedha, kodi, teknolojia ya habari na mawasiliano, ununuzi, ujasiriamali, uchumi na fani nyengine zinazohusiana kama itakavyoamuliwa na Baraza;

(e) kushirikiana na taasisi za kitaifa, kikanda na kimataifa katika kuendeleza elimu, utafiti, ubunifu au viwango vya kimataifa vya masuala ya fedha;

(f) kufanya utafiti na kutoa huduma za ushauri na ushauri elekezi;

(g) kuendesha na kusimamia mitihani kwa ajili ya kutathmini uwezo na umahiri wa wanafunzi;

(h) kutoa shahada, stashahada, astashahada na tuzo nyengine za kitaaluma kama zitakavyoidhinishwa na Baraza; na

(i) kufanya kazi nyengine yoyote kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii.

Mafunzo maalumu ya vitendo.

**6.** Kutakuwa na mafunzo maalumu ya vitendo kwa wanafunzi ambayo yatatolewa kwa kuzingatia fani ya masomo husika katika maeneo kama itakayoamuliwa na Chuo.

## SEHEMU YA TATU
## UENDESHAJI NA USIMAMIZI WA CHUO

Baraza la Chuo.

**7.-**(1) Kutakuwa na Baraza la Chuo ambalo litaundwa na:

(a) Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais;

(b) Mkuu wa Chuo;

(c) Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Wahasibu, Wakaguzi na Washauri Elekezi wa Kodi Zanzibar;

(d) Muhasibu Mkuu wa Serikali;

(e) Mkuu wa Serikali ya Wanafunzi;

(f) Wakili wa Serikali kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu; na

(g) mjumbe mmoja kutoka:

(i) Wizara inayohusika na elimu;

(ii) taasisi ya elimu ya juu; na

(iii) taasisi ya sekta binafsi.

(2) Wajumbe chini ya kifungu kidogo cha (1)(f) na (g) cha kifungu hiki, watateuliwa na Waziri kwa kushauriana na wakuu wa taasisi husika kwa kuzingatia jinsia, uzoefu na taaluma zao.

Sifa za Mwenyekiti.

**8.** Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Baraza ikiwa mtu huyo ana:

(a) angalau shahada ya pili katika fani ya fedha au fani nyengine yoyote inayohusiana kutoka katika taasisi inayotambuliwa na Serikali;

(b) uzoefu wa kazi wa angalau miaka kumi katika sekta ya umma au binafsi; na

(c) uadilifu wa hali ya juu.

Kazi za Baraza.

**9.** Baraza litakuwa na kazi ya:

(a) kusimamia utendaji wa jumla wa Chuo;

(b) kusimamia matumizi ya fedha na mali za Chuo;

(c) kutoa maelekezo ya jumla kwa ajili ya usimamizi bora na wa ufanisi wa Chuo;

(d) kuimarisha na kulinda ustawi na maslahi ya wanafunzi na wafanyakazi wa Chuo; na

(e) kufanya kazi nyengine yoyote kwa ajili ya utekelezaji wa masharti ya Sheria hii.

Uwezo wa Baraza.

**10.** Baraza litakuwa na uwezo wa:

(a) kupitia na kuidhinisha ripoti za Chuo;

(b) kuidhinisha mitaala, astashahada, stashahada, shahada na tuzo nyengine zinazotolewa na Chuo;

(c) kuidhinisha udahili wa wanafunzi;

(d) kuidhinisha matokeo ya mitihani ya Chuo;

(e) kuidhinisha ada za masomo na tozo za huduma zinazotolewa na Chuo;

(f) kupendekeza muundo wa utumishi wa Chuo;

(g) kuajiri, kupandisha daraja na kuteua wafanyakazi wa Chuo kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011; na

(h) kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya wafanyakazi wa Chuo.

Katibu wa Baraza.

**11.-**(1) Baraza litateua mfanyakazi wa Chuo kuwa Katibu wa Baraza.

(2) Mfanyakazi wa Chuo atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Katibu wa Baraza ikiwa mtu huyo ana:

(a) angalau shahada ya kwanza katika fani ya sheria au ana sifa ya kuwa katibu wa shirika kutoka katika taasisi inayotambuliwa na Serikali;

(b) uzoefu wa kazi wa angalau miaka mitano katika utumishi wa umma; na

(c) uadilifu wa hali ya juu.

(3) Katibu wa Baraza atawajibika kwa Baraza na:

(a) kwa kushauriana na Mwenyekiti, ataandaa ajenda za vikao vya Baraza;

(b) atachukua kumbukumbu sahihi za vikao vya Baraza;

(c) atatunza kumbukumbu sahihi na zenye kujitosheleza za vikao vya Baraza;

(d) atatoa taarifa sahihi za vikao vya Baraza kwa wajumbe; na

(e) atatekeleza kazi nyengine yoyote kama atakavyoelekezwa na Baraza.

Mwenendo wa vikao vya Baraza.

**12.** Masharti yanayohusiana na mwenendo wa vikao vya Baraza yatakuwa kama yalivyoainishwa katika Jadweli la Sheria hii.

Uteuzi wa Mkuu wa Chuo.

**13.-**(1) Kutakuwa na Mkuu wa Chuo ambaye atateuliwa na Rais kwa njia ya ushindani wa kuajiri kwa mujibu wa masharti kama Rais atakavyoamua.

(2) Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Mkuu wa Chuo ikiwa mtu huyo ana:

(a) shahada ya uzamivu katika fani ya fedha, uchumi, biashara au fani nyengine yoyote inayohusiana kutoka katika taasisi inayotambuliwa na Serikali;

(b) uzoefu wa kazi wa angalau miaka saba katika sekta ya umma au binafsi; na

(c) uadilifu wa hali ya juu.

Kazi za Mkuu wa Chuo.

**14.-**(1) Mkuu wa Chuo atakuwa ni Afisa Mtendaji Mkuu wa Chuo na atawajibika kwa shughuli za kila siku za Chuo.

(2) Bila ya kuathiri ujumla wa kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mkuu wa Chuo atakuwa na kazi zifuatazo:

(a) kusimamia nidhamu ya wakufunzi, wanafunzi na wafanyakazi wa Chuo;

(b) kutekeleza na kuhakikisha utekelezaji wa uamuzi wa Baraza;

(c) kusimamia masuala ya kitaaluma na maendeleo ya Chuo;

(d) kukuza na kuimarisha mashirikiano baina ya Chuo na taasisi nyengine za elimu ndani na nje ya Zanzibar;

(e) kuandaa na kuwasilisha bajeti ya mwaka kwa Baraza;

(f) kuandaa ripoti ya Chuo kwa mujibu wa maelekezo ya Baraza; na

(g) kufanya kazi nyengine yoyote kama atakavyoelekezwa na Baraza kwa mujibu wa sheria.

Uteuzi wa Naibu Mkuu wa Chuo Utawala, Mipango na Fedha.

**15.-**(1) Kutakuwa na Naibu Mkuu wa Chuo Utawala, Mipango na Fedha ambaye atateuliwa na Rais kwa njia ya ushindani wa kuajiri kwa mujibu wa masharti kama Rais atakavyoamua.

(2) Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Naibu Mkuu wa Chuo Utawala, Mipango na Fedha ikiwa mtu huyo ana:

(a) shahada ya uzamivu katika utawala wa umma, au fani nyengine yoyote inayohusiana kutoka katika taasisi inayotambuliwa na Serikali;

(b) uzoefu katika masuala ya utawala kwa muda usiopungua miaka saba; na

(c) uadilifu wa hali ya juu.

Kazi za Naibu Mkuu wa Chuo Utawala, Mipango na Fedha.

**16.-**(1) Naibu Mkuu wa Chuo Utawala, Mipango na Fedha atakuwa msaidizi na mshauri mkuu wa Mkuu wa Chuo katika masuala yanayohusiana na utawala, mipango na fedha za Chuo:

(2) Bila ya kuathiri ujumla wa kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Naibu Mkuu wa Chuo Utawala, Mipango na Fedha atakuwa na kazi zifuatazo:

(a) kusimamia utekelezaji wa mpango mkakati pamoja na miongozo inayotolewa na Chuo kuhusiana na utawala, mipango na fedha;

(b) kusimamia masuala yote yanayohusiana na utawala kama atakavyoelekezwa na Baraza;

(c) kuwezesha uteuzi wa wafanyakazi wenye sifa na uwezo wa hali ya juu kwa ajili ya kuboresha utendaji kazi;

(d) kufanya tathmini ya utendaji kazi na kutoa mrejesho wa wafanyakazi;

(e) kuandaa programu za mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwa wafanyakazi; na

(f) kufanya kazi nyengine yoyote kama atakavyoelekezwa na Baraza kwa mujibu wa Sheria.

Uteuzi wa Naibu Mkuu wa Chuo Taaluma, Utafiti na Ushauri Elekezi.

**17.-**(1) Kutakuwa na Naibu Mkuu wa Chuo Taaluma, Utafiti na Ushauri Elekezi ambaye atateuliwa na Raiskwa njia ya ushindani wa kuajiri kwa mujibu wa masharti kama Rais atakavyoamua.

(2) Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Naibu Mkuu wa Chuo Taaluma, Utafiti na Ushauri Elekezi ikiwa mtu huyo ana:

(a) shahada ya uzamivu katika fani ya uchumi, fedha, uhasibu au fani nyengine yoyote inayolingana kutoka katika taasisi inayotambuliwa na Serikali;

(b) uzoefu katika masuala ya taaluma kwa muda usiopungua miaka saba; na

(c) uadilifu wa hali ya juu.

Kazi za Naibu Mkuu wa Chuo Taaluma, Utafiti na Ushauri Elekezi.

**18.-**(1) Naibu Mkuu wa Chuo Taaluma, Utafiti na Ushauri Elekezi atakuwa msaidizi na mshauri mkuu wa Mkuu wa Chuo katika masuala ya taaluma, utafiti, ushauri elekezi na utaalamu wa Chuo.

(2) Bila ya kuathiri ujumla wa kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Naibu Mkuu wa Chuo Taaluma, Utafiti na Ushauri Elekezi atakuwa na kazi zifuatazo:

(a) kutekeleza masuala yote ya kitaaluma kama atakavyoelekezwa na Baraza;

(b) kusimamia masuala yote yanayohusiana na usajili wa wanafunzi;

(c) kuhakikisha udhibiti wa ubora na viwango vya kitaaluma;

(d) kuandaa na kusimamia mafunzo ya kitaaluma ya muda mrefu na muda mfupi, huduma za ushauri elekezi na utafiti;

(e) kuwasilisha matokeo ya mitihani kwa Uongozi wa Chuo na kwa Baraza;

(f) kusimamia utekelezaji wa mpango mkakati pamoja na miongozo inayotolewa na Chuo kuhusiana na masuala ya kitaaluma, utafiti na ushauri elekezi; na

(g) kufanya kazi nyengine yoyote kama atakavyoelekezwa na Baraza kwa mujibu wa Sheria.

Muda wa Mkuu wa Chuo na Naibu Wakuu wa Chuo.

**19.** Mkuu wa Chuo na Naibu Wakuu wa Chuo watashika nafasi kwa kipindi cha miaka mitatu na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine kimoja tu.

Idara, vitengo na divisheni.

**20.-**(1) Chuo kinaweza kuanzisha idara, vitengo na divisheni kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011.

(2) Wakuu wa idara na vitengo watateuliwa na Baraza kwa kuzingatia sifa na uzoefu wao.

(3) Wakuu wa divisheni watateuliwa na Mkuu wa Chuo kwa kuzingatia sifa na uzoefu wao.

(4) Wakuu wa idara, vitengo na divisheni watawajibika kwa Mkuu wa Chuo.

Wafanyakazi wa Chuo.

**21.** Kutakuwa na wafanyakazi wa Chuo ambao wataajiriwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011.

Serikali ya wanafunzi.

**22.** Kutakuwa na Serikali ya Wanafunzi ya Chuo ambayo itaanzishwa kwa mujibu wa katiba itakayoidhinishwa na Baraza.

## SEHEMU YA NNE
## MASHARTI YA FEDHA

Fedha na rasilimali za Chuo.

**23.-**(1) Fedha na rasilimali za Chuo zitajumuisha:

(a) fedha zitakazoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi;

(b) ada au tozo zinazokusanywa na Chuo;

(c) ruzuku, zawadi, misaada, michango au mkopo kama Chuo kitakavyopokea kutoka kwa mtu au taasisi yoyote; na

(d) fedha nyengine zozote zinazoweza kupatikana kihalali na Chuo.

(2) Miamala yote ya fedha ya Chuo itafanywa na itasimamiwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam.12 ya 2016.

Bajeti ya Chuo.

**24.-**(1) Mkuu wa Chuo, katika kila mwaka wa fedha, ataandaa na atawasilisha kwa Baraza kwa ajili ya majadiliano na mapendekezo makadirio ya kina ya mapato na matumizi ya Chuo kwa mwaka wa fedha unaofuata.

(2) Baada ya majadiliano na mapendekezo ya Baraza, bajeti ya Chuo itachukuliwa kuwa sehemu ya bajeti ya Wizara.

(3) Makadirio ya mapato na matumizi ya Chuo yataandaliwa kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam.12 ya 2016 na miongozo mengine yoyote kama itakavyoweza kutolewa na Serikali kila baada ya muda.

(4) Mkuu wa Chuo atahakikisha kwamba malipo yote yanayofanywa kwa fedha za Chuo yanafanywa kwa usahihi na yanaidhinishwa ipasavyo na udhibiti wa kutosha unadumishwa juu ya mali na madeni ya Chuo.

Hesabu na ukaguzi.

**25.-**(1) Chuo kitaweka na kitatunza kwa usahihi vitabu vya hesabu ambavyo vinajumuisha kumbukumbu zote za fedha na miamala kwa kila mwaka wa fedha.

(2) Taarifa za fedha za mwaka za Chuo zitakaguliwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam. 12 ya 2016 na sheria nyengine zozote za fedha zinazohusika.

Kufungua hesabu za benki.

**26.** Chuo, kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam.12 ya 2016 kitafungua hesabu za benki kwa ajili ya utekelezaji bora wa kazi zake.

Ripoti ya Utekelezaji ya mwaka.

**27.** Mkuu wa Chuo, ndani ya miezi mitatu baada ya mwisho wa kila mwaka wa fedha, ataandaa na atawasilisha kwa Waziri ripoti ya utekelezaji ya mwaka katika kila mwaka huo wa fedha, kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha, Nam. 12 ya 2016 na sheria nyengine yoyote ya fedha inayohusika.

Uwezo wa kuwekeza.

**28.** Chuo kitakuwa na uwezo wa kuwekeza fedha zake katika uwekezaji ambao una faida, salama na halali kwa mujibu wa sheria husika.

## SEHEMU YA TANO
## MASHARTI MENGINEYO

Kamati ya Nidhamu.

**29.-**(1) Kutakuwa na Kamati ya Nidhamu ya Wanafunzi ambayo itasikiliza, itaamua na itachunguza masuala ya kinidhamu yanayomuhusu mwanafunzi wa Chuo.

(2) Muundo, taratibu na mambo mengine yanayohusiana na Kamati ya Nidhamu ya Wanafunzi yataainishwa katika kanuni.

Rufaa.

**30.** Mwanafunzi ambaye hajaridhika na uamuzi wa Kamati ya Nidhamu ya Wanafunzi anaweza kukata rufaa kwa Baraza kwa mujibu wa taratibu kama zitakavyoelezwa katika kanuni.

Kanuni.

**31.-**(1) Waziri anaweza kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Waziri anaweza kutunga kanuni kuhusiana na:

(a) taratibu za utoaji wa tuzo yoyote chini ya Sheria hii;

(b) uendeshaji wa mitihani;

(c) ada na tozo zinazolipwa chini ya Sheria hii;

(d) taratibu za kinidhamu dhidi ya mwanafunzi; na

(e) programu za mafunzo zitakazotolewa na Chuo.

## JADWELI

## MWENENDO WA VIKAO VYA BARAZA
**[Chini ya kifungu cha 12]**

Makamu Mwenyekiti.

**1.** Wajumbe wa Baraza, watamchagua mjumbe mmoja miongoni mwao kuwa Makamu Mwenyekiti.

Muda wa wajumbe.

**2.** Isipokuwa wajumbe wanaoingia kwa nafasi zao, Mwenyekiti na wajumbe wengine wa Baraza, watashika nafasi kwa kipindi cha miaka mitatu kutoka tarehe ya uteuzi wao na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine kimoja tu.

Vikao vya Baraza.

**3.-**(1) Baraza litakutana mara moja kila baada ya miezi mitatu na inaweza kukutana katika vikao vya dharura wakati wowote itakapohitajika kwa ajili ya kutekeleza kazi zake.

(2) Vikao vyote vya Baraza vitaendeshwa na Mwenyekiti, na ikiwa hayupo vitaendeshwa na Makamu Mwenyekiti na ikiwa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wote hawapo, wajumbe waliopo watamchagua mmoja miongoni mwao kuongoza kikao.

Akidi.

**4.** Zaidi ya idadi nusu ya wajumbe watawunda akidi katika kikao chochote cha Baraza.

Uamuzi wa Baraza.

**5.** Uamuzi wa Baraza utafanywa kwa makubaliano, endapo hakutakuwa na makubaliano, uamuzi utafanywa kwa kura na iwapo kura zitakuwa sawa, Mwenyekiti atakuwa na kura ya uamuzi.

Taratibu za vikao.

**6.** Baraza litakuwa na uwezo wa kuandaa taratibu zake zenyewe kuhusiana na vikao.

Mjumbe mualikwa.

**7.** Baraza linaweza kumualika mtu yeyote kushiriki majadiliano yoyote ya kikao cha Baraza kama mtaalamu lakini mtu huyo aliyealikwa hatokuwa na haki ya kupiga kura.

Kumbu-kumbu za vikao vya Baraza.

**8.** Kumbukumbu za vikao vya Baraza zitathibitishwa na Baraza katika kikao kinachofuata na kusainiwa na Mwenyekiti na Katibu.

Kamati ya Baraza.

**9.** Baraza linaweza, kwa madhumuni ya kuwezesha utekelezaji wa kazi zake, kuanzisha kamati kama itakavyoona inafaa.

Kukasimu kazi za Baraza.

**10.-**(1) Baraza linaweza, pale litakapoona inafaa kwa ajili ya utekelezaji bora wa kazi zake, kukasimu baadhi ya kazi zake kwa Kamati ya Baraza.

(2) Endapo Baraza litakasimu kazi zake chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, litatoa miongozo kwa maandishi endapo itahitajika ili kuhakikisha utekelezaji mzuri wa kazi hizo.

Kubainisha maslahi.

**11.-**(1) Mjumbe wa Baraza ambaye ana maslahi ya moja kwa moja au vyenginevyo juu ya jambo linalohusika au linalotakiwa kujadiliwa na Baraza, haraka iwezekanavyo baada kutambua, atabainisha uhalisia wa maslahi yake mwanzoni mwa kikao cha Baraza.

(2) Ubainishaji wa maslahi chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, utawekwa katika kumbukumbu za kikao na mjumbe aliyebainisha maslahi:

(a) hatahudhuria katika majadiliano ya Baraza kwa ajili ya kufanya uamuzi; au

(b) hatamshawishi mjumbe mwengine yeyote katika kufanya uamuzi.

Kusita kuwa mjumbe.

**12.** Mjumbe atasita kushika nafasi ikitokea moja kati ya yafuatayo:

(a) amejiuzulu;

(b) ikiwa hatahudhuria vikao vitatu mfululizo vya Baraza bila ya kuwa na sababu za msingi;

(c) ikiwa atashindwa kutekeleza kazi zake kwa sababu za afya ya kimwili au kiakili;

(d) ikiwa atasita kuwa mwakilishi wa taasisi iliyompendekeza mjumbe huyo;

(e) ikiwa atasitishwa na Waziri kwa kushindwa kutimiza matarajio ya Chuo; au

(f) kifo.

Posho la wajumbe wa Baraza.

**13.** Mwenyekiti na wajumbe wengine wa Baraza watastahiki kulipwa posho kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011.

## MADHUMUNI NA SABABU

Madhumuni ya Mswada huu ni kuanzisha Chuo cha Fedha Zanzibar kama Chuo huru na kuweka mfumo wa kisheria na kitaasisi kwa ajili ya usimamizi na uendeshaji wa Chuo, kufuatia kuingizwa kwa kilichokua Chuo cha Uongozi wa Fedha Zanzibar katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar na kupotea kwa hadhi yake ya kisheria ya kujitegemea.

Mswada huu unakusudia kurejesha na kuimarisha uwezo wa Chuo katika kutoa elimu na mafunzo ya kitaalamu, huduma za ushauri elekezi na kujenga uwezo katika fani za fedha, uchumi, kodi, bima, benki, ununuzi, uhasibu, masoko ya mitaji, dhamana na fani nyengine zinazohusiana, ili kukidhi mahitaji ya kitaifa ya wataalamu wenye ujuzi.

Aidha, Mswada huu unakusudia kuimarisha mamlaka ya Chuo katika utoaji na udhibiti wa elimu na mafunzo kwa kuweka masharti kuhusu uandaaji na mapitio ya mitaala na programu za mafunzo, mafunzo ya vitendo, mitihani na utoaji wa tuzo za kitaaluma, kwa madhumuni ya kuhakikisha kuwa elimu na mafunzo yanayotolewa yanaendana na mahitaji yanayobadilika ya sekta za fedha na sekta zinazohusiana.

Mswada huu pia unakusudia kukuza ushirikiano kati ya Chuo na taasisi za kitaifa, kikanda na kimataifa katika elimu, utafiti, ubunifu na maendeleo ya kitaaluma, na kukiwezesha Chuo kuchangia katika kuimarisha uzalishaji na ufanisi katika usimamizi wa rasilimali za kifedha.

Mswada huu umegawika katika Sehemu Tano:

***Sehemu ya Kwanza:*** Sehemu hii inahusiana na masharti ya awali yanayojumuisha jina fupi na kuanza kutumika kwa Sheria na ufafanuzi wa maneno yaliyotumika katika Sheria kwa madhumuni ya kutoa ufasaha wa maneno ambayo yanaweza kusababisha utata.


***Sehemu ya Pili:*** Sehemu hii inaweka masharti ya uanzishwaji, hadhi ya kisheria na kazi za Chuo ambazo zinajumuisha kufanya utafiti na kutoa huduma za ushauri elekezi pamoja na mafunzo maalumu ya vitendo. Sehemu hii ni muhimu kwani inakipa Chuo mamlaka ya kisheria yanayohitajika ili kutekeleza kazi zake.

***Sehemu ya Tatu:*** Sehemu hii inaweka masharti ya usimamizi na uendeshaji wa Chuo. Inaweka masharti ya uanzishwaji, muundo na mambo mengine yanayohusu Baraza, uteuzi, sifa na kazi za Mkuu wa Chuo na Naibu Wakuu wa Chuo, unzishwaji wa idara, vitengo na divisheni za Chuo pamoja na Serikali ya Wanafunzi. Masharti haya yanaweka mfumo madhubuti wa utawala na usimamizi wa Chuo.

Sehemu hii inaelezea masuala ya fedha ya Chuo, ikijumuisha vyanzo vya fedha na rasilimali, bajeti, hesabu na ukaguzi, kufungua hesabu za benki, taarifa ya utendaji ya mwaka na uwekezaji kwa madhumuni ya kuhakikisha usimamizi bora wa fedha, uwajibikaji na uendelevu wa kifedha.

***Sehemu ya Tano:*** Sehemu hii inaweka masharti mengineyo ambayo yanalenga kuelezea mashauri ya kinidhamu dhidi ya wanafunzi, haki ya kukata rufaa na uwezo wa Waziri kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji wa masharti ya Sheria,

Mwisho, kuna Jadweli linaloweka masharti kuhusu mwenendo wa vikao vya Baraza kwa madhumuni ya kuhakikisha utekelezaji wa kazi za Baraza kwa utaratibu na ufanisi.



**ZANZIBAR.** **(DKT. JUMA MALIK AKILI)**
**18 Agosti, 2026** **WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO**

**LIMEPIGWA CHAPA NA WAKALA WA SERIKALI WA UCHAPAJI ZANZIBAR 2026**